# Changamoto Zinazomkabili Mhusika wa Kiume katika Riwaya ya *Nguu za Jadi*

**1.Agnes Mwongeli Kiema, 1. John Mutua, 2. Sarah Ndanu Ngesu**

Agnesmwongeli05@gmail.com john.mutua@mksu.ac.ke sngesu@seku.ac.ke
0708825097 0721358133 0722866041
1 Machakos University
2 South Eastern Kenya University.
https://orcid.org/0009-0007-9135-9121

**Ikisiri**

Makala hii imebainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya ya Clara Momanyi; *Nguu za Jadi* (2021). Katika enzi zetu mwanamke amewekwa mbele kinyume na ilivyokuwa wakati dunia ilikuwa imetawaliwa na ubabedume. Inaonekana kana kwamba mambo yamebadilika. Mabadiliko haya yamemwathiri mwanamume katika jamii. Tafiti nyingi za hapo awali zinaonekana kuegemea zaidi kwenye aina za dhuluma zinazowakumba wanawake katika jamii za Kiafrika. Jambo hili linaathiri jamii kwa kuipa mtazamo kuwa, jinsia ya kiume haikabiliwi na matatizo yoyote. Makala hii iliogozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia ya uhalisia inadai kwamba, fasihi inatakiwa kutoa picha halisi ya jamii husika. Nadharia hii ilizuka huko Ulaya katika karne ya kumi na tisa. Makala hii itatoa mwanga mkubwa kuhusiana na masuala ya jinsia ya kiume. Aidha, utafiti huu utakuwa kichocheo cha watafiti wa baadaye wa fasihi kuchunguza masuala yanayohusu jinsia ya kiume. Halikadhalika, kutokana na makala hii, jamii itaweza kubaini changamoto mbalimbali zinazoikabili jinsia ya kiume na athari ya changamoto hizo na hivyo itabuni mikakati ya kukabiliana nazo.

**Maneno Muhimu**: changamoto, mhusika, jinsia, nadharia, uhalisia na fasihi

**Utangulizi**

Jinsia ni suala mtambuko ambalo linaendelea kuwashughulisha wataalamu wengi duniani. Bayyo (2020) anaeleza kuwa, katika mjadala kuhusiana na masuala ya jinsia, fikra za watu wengi huelekea kwa jinsia ya kike. Jinsia ya kike hupewa kipaumbele kwa kujadiliwa na kuoneshwa namna inavyoonewa na kudhulumiwa. Suala hili limekuwa likiendelea kiasi cha kuaminika kuwa jinsia ya kiume haikabiliwi na matatizi yoyote, bali hulaumiwa kwa matatizo yanayoikabili jinsia ya kike.

Atieno (2019) anaeleza kuwa, jamii imepuuza jinsia ya kiume kutokana na fikra kuwa ina uwezo wa kujitetea na kukabiliana na changamoto inayokumbana nazo. Jambo hili limechangia hali yao ya upweke kwa sababu hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Atieno anaendelea kusema kuwa, Wafeministi wa Kiafrika wanaopigania ukombozi wa mwanamke, haki na usawa wa kijinsia, wamenuia kuwapa wanawake mwelekeo mbadala kwa msingi wa utamaduni wa kimapokeo ilhali wanaume wamesalia kufuata mwelekeo wa kimapokeo kwa kukosa mwelekeo mbadala kama wanawake, jambo ambalo linaathiri uhusiano wao zaidi.

Msukumo wa kuichagua mada hii umetokana na kuwepo kwa pengo katika kuchunguza masuala ya jinsia ya kiume. Isitoshe, baadhi ya watafiti walipendekeza tafiti zifanywe ili kuangalia upande wa pili wa masuala ya kijinsia kwa sababu mengi yametafitiwa kuhusiana na jinsia ya kike. Watafiti hawa ni kama Momanyi (1998), Kimani (2003), King'ei (2002) na Wandera (2002) ambao wanaeleza kuwa, tafiti za kijinsia katika fasihi ya Kiswahili bado zitaendelea kuwepo kwa sababu binadamu anaendelea kuwepo. Makala hii imebainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya ya *Nguu za Jadi*.

**Nadharia ya Uhalisia**

Makala hii iliongozwa na nadharia ya uhalisia. Kulingana na maelezo ya Mbatia (2001:92), uhalisia ni tapo la uandishi lililozuka huko Ulaya katika karne ya kumi na nane (18) na kusambaa katika mataifa mengine ya ulimwengu. Msingi wa tapo hili uliwekwa na mwanafalsafa anayejulikana kama Hegel katika kitabu chake cha *Aesthetics* (Ujumi). Mwanafalsafa huyu alipendekeza matumizi ya "uhalisia" yaeleze kazi ya kifasihi inayouwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa

jinsi inavyochochewa waziwazi na hali aliyomo, Wamitila (2002). Mulokozi (2017) anasema ya kwamba fasihi iyasawiri maisha kama yalivyo bila kupotosha wala kutia chumvi huku ikijikita katika kuonyesha mahusiano na migongano ya kijamii, matatizo na pia matamanio ya mtu wa kawaida ndani ya jamii.

**Matokeo ya utafiti**

Kupitia riwaya ya *Nguu za Jadi,* tumebaini changamoto mbalimbali ambazo, jinsia ya kiume hukumbana nazo katika maisha ya kila siku. Changamoto hizo zimejadiliwa katika sehemu hii. Nazo ni; ukosefu wa ajira, ukosefu wa matumaini, kutelekezwa katika jamii, ulevi wa pombe na malezi mabaya.

**Ukosefu wa ajira**

Ajira ni kazi ambayo mtu huifanya ili kulipwa mshahara. Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, vijana wengi wa jamii ya Waketwa hata waliosoma wanaonekana kukosa ajira. Inaelezwa kuwa, kutokana na uongozi mbaya wa Mtemi Lesulia uliojaa ufisadi na ukabila, vijana wengi wa kiume hata wale waliohitimu katika taaluma mbalimbali walikosa ajira. Baadhi yao walianza kushikilia kwamba elimu haikuwa na thamani kwao. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Ukosefu wa ajira hasa kwa vijana waliolitimu katika taaluma mbalimbali ulikuwa sasa ni mazoea (uk.44).

Mwandishi anasema kuwa, nchi ya Matuo ilishindwa kupanua uchumi ili kuwaajiri vijana wa kiume, na haikuweza kuanzisha miradi ya kuwawezesha kujiinua kiuchumi. Hata hivyo, kazi zilizopatikana zilipewa watu wasiokuwa na ujuzi wala maarifa, jambo ambalo linapelekea maendeleo ya nchi kukwama na maafa mengi kutokea. Inaelezwa pia kuwa, kazi zilizokuwepo zilipeanwa kwa kujuana hata kama mtu hakuhitimu ipasavyo. Hivyo basi, vijana wa kiume wa jamii ya waketwa wakabaki kuhangaika mijini. Mwandishi anasema:

> Vijana wengi Waketwa waliohitimu shahada za vyuo vikuu walihangaika mjini kutafuta kazi bila mafanikio katika majopo ya uajiri, utawala ulihakikisha kwamba hawa hawaajiriwi katika kazi zilizokuwa na mamlaka ya uongozi (uk.44).

Mtunzi amefanikiwa kuonyesha hali halisi ilivyo katika jamii ya sasa. Changamoto hii ya ukosefu wa ajira imewakumba vijana wengi wa kiume katika jamii ya sasa. Hivyo, mwandishi kupitia riwaya hii ameweza kueleza mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha.

**Ukosefu wa matumaini**

Mwandishi wa riwaya hii amemchora mhusika wa kiume kama mtu aliyekosa matumaini katika maisha. Ukosefu wa matumaini unabainika pale ambapo, idadi kubwa ya vijana wa kiume inaonekana kuzurura mjini na kupoteza wakati wao katika viambaza vya maduka. Mwandishi anasema:

> Ukosefu wa matumaini ya kuishi ulianza kuhasiri mifumo ya kijamii. Asasi ya familia ikaathirika sana pale mizozano ya kifamilia ilipokithiri (uk.47).

Inaelezwa kuwa, Mangwasha alikuwa akiwaonea huruma vijana hawa ambao aliwaona kama kizazi kilichopotea kama tunavyoambiwa na mwandishi kuwa:

> Mangwasha aliwaona kama kizazi kilichopotea. Je, hawa wangeweza kuwa raia wa kuaminiwa kesho kweli? (uk.34).

Inaelezwa kuwa, vijana wengine walizurura tu katika barabara za mji wasijue wafanyalo. Maneno ya mwandishi yanadhihirisha wazi ukosefu wa matumani kwa vijana wa kiume kama anavyoonyesha kupitia kinywa cha Mangwasha kuwa:

> “Hawa watakuwa wanaume wenye kutunza jamaa zao kweli? (uk.49).

Aidha, mwandishi anaonyesha kuwa, changamoto ya ukosefu wa matumaini miongoni mwa wahusika wa kiume katika riwaya hii imetokana na kutelekezwa kwa jinsia ya kiume. Mangwasha anasema kuwa, kuna maandiko mengi yanayomwelekeza mtoto wa kike jinsi ya kuishi ilhali ni machache yanayomfunza mtoto wa kiume. Anasema kuwa, vijana wengi wa kiume hukumbana na mauti katika harakati za kujaribu kuwa wanaume. Inaelezwa kuwa, hakuna dira ya kumuongoza mtoto wa kiume jambo ambalo linampelekea kukosa matumaini maishani. Kupitia kinywa cha Mangwasha mwandishi anasema kuwa:

> Ole wako ewe mwanaume uishiye leo, unayechakura mapipa ili kuzimia njaa. Uliikosea nini jamii hata usalie kuwa ombaomba? Umevaa koti kuukuu na umesalia kuwa nyuma kama koti hilo mwanetu (uk.138).

Ukosefu wa matumaini ni changamoto ambayo huikumba jinsia ya kiume katika maisha ya kila siku katika jamii halisi. Kupitia riwaya hii, Clara Momanyi ameonyesha uhalisia uliopo katika jamii. Maoni ya mtafiti ni kuwa, hatua ichukuliwe ili kukiokoa kizazi cha kiume kinachopotea nyikani kwa kukosa matumaini.

**Kutelekezwa katika jamii**

Mhusika wa kiume katika riwaya hii anaonekana kutelekezwa, yaani amepuuzwa ama hakuna anayemjali katika jamii. Mhusika wa kiume anaonekana kutoshughulikiwa jinsi ambavyo mhusika wa kike anashughulikiwa. Mwandishi anaeleza kuwa, Mangwasha amekuwa akipitia maandiko mengi ambayo yanamfunza mtoto wa kike jinsi ya kuwa mwanamke, lakini amegundua kuwa maandiko yanayomuelekeza mtoto wa kiume jinsi ya kuishi ni machache mno. Inaelezwa kuwa, vijana wengi wa kiume hukumbana na changamoto za aina nyingi na hata mauti katika kujaribu kuwa wanaume. Mtoto wa kiume amekosa dira ya kumwongoza. Maneno haya yanadhihirisha kuwa mhusika wa kiume ametelekezwa katika jamii ya Matuo. Mwandishi anasema:

> Hakuna dira mahususi ya kumwongoza mtoto wa kiume. Dira hiyo ni mzazi wake wa kiume. Aghalabu huyu hayuko au hata hajulikani. Hivyo hapati mafunzo yoyote kutoka kwake (uk.138).

Maneno haya ni dhihirisho wazi kuwa mhusika wa kiume katika riwaya hii hana mtu wa kumwelekeza. Ametelekezwa. Inaonekana kuwa, mwanamume katika familia ndiye dira inayofaa kumwelekeza mtoto wake wa kiume ila hayupo, au hata akiwepo, ana kazi nyingine za kufanya. Tunaona kuwa mzazi wa kiume katika jamii hii hana wasaa wa kumwelekeza mwanawe wa kiume, hali ambayo inampelekea kukumbwa na changamoto za aina nyingi. Mwandishi kupitia mawazo ya Mangwasha anasema:

> "Ole wako mwanamume uishiye leo. Unayechakura mapipa ili kuizima njaa. Uliikosea nini jamii hata usalie kuwa ombaomba…yu wapi baba aliyekutelekeza? Iwapi jamii isiyodhamini elimu na utu wako? Jamii ilimshika mkono mtoto wa kike. Ikasahau kwamba hata wewe unastahili kushikwa mkono (uk.138).

Aidha tunaona kuwa, Lonare anapochaguliwa kuwa Mtemi wa Nchi ya Matuo, ana lengo la kubadilisha maisha ya vijana wa kiume ambao anawaona kuwa wametengwa na jamii na wanapitia changamoto za aina mbalimbali. Kupitia kinywa cha Lonare, mwandishi anasema;

> Aidha, serikali yangu itadhibiti ujasiriamali miongoni mwao kwa njia mbalimbali. Hii ni kwa sababu tegemeo la vijana ndio tegemeo la matuo la baadaye. Jamii hii imewatenga sana vijana wa kiume. Je, familia zitajengwaje ikiwa mume haonekani kuwa mume ndani ya nyumba? (uk.180).

Hali ilivyo ndani ya riwaya hii ndivyo inavyoonekana katika jamii halisi. Nadharia ya uhalisia inadai ya kwamba, fasihi ieleze mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Katika jamii ya sasa mwanaume ametelekezwa, amepuuzwa na kutengwa huku mwanamke akipewa kipaumbele katika jamii. Katika katiba ya Kenya (2010) kifungu cha tisini na saba (97), kila eneo eneo bunge lina mwakilishi wa wanawake ilhali hakuna anayewakilisha wanaume. Atieno (2019) anasema kuwa tafiti kadha za hapo awali zimeshughulikia masuala ya wanawake na kupuuzwa kwa masuala ya wanaume. Anasema kuwa, hali ya wanaume imekuwa ya upweke kwa sababu hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama invyofanyiwa jinsia ya kike. Msimamo wa mtafiti ni kwamba, wanaume na wanawake wapewe nafasi sawa katika jamii.

**Ulevi wa pombe**

Mtafiti wa kazi hii amebaini kuwa, ulevi wa pombe ni mojawapo ya changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya hii na inapelekea kutofaulu kupata maendeleo katika jamii zao. Changamoto ya ulevi inadhihirishwa na mhusika Mrima anayeiacha familia yake na kushiriki ulevi kupitia kwa Sagilu. Mwandishi anatuonyesha haya kupitia kinywa cha Mangwasha kuwa:

> Mrima haonekani kujitwika majukumu yake ya unyumba tena. Anakesha na kuamkia ulevini. Hana habari tena kuhusu familia yake. (uk.29).

Aidha tunaona kuwa, wakati Mangwasha anaondoka kuelekea Ponda Mali kumtafuta mumewe aliyepotelea ulevini, anapata kujionea jinsi changamoto hii ya ulevi ilivyowalemea wanaume katika jamii yao. Mwandishi anasema:

> Njiani alikumbana na walevi waliozua vitimbi vya kila aina. Wengine waliimba nyimbo zisizokuwa na mahadhi ilhali wengine walibaki kutoa

> vicheko vilivyowaudhi wapita njia. Hapa na pale aliwaona wengine wakitapika ovyo baada ya nishai za ulevi kunoga. (uk.34).

Isitoshe, pale Majaani ambapo Mrima aliokotwa palijaa walevi waliolewa chakari. Hii ni kumaanisha kuwa, changamoto ya ulevi imewalemea wahusika wengi wa kiume katika riwaya hii. Mwandishi anaeleza:

> Hapa palikuwa na walevi waliolewa chakari. Baadhi yao walikuwa wanavuta sigara. Wengine waliendelea kubugia pombe kutoka katika chupa walizobeba. Wengine tayari walikuwa wametekwa na usingizi. Walilala vinywa wazi bila kujali nzi waliong'ong'a nyuso zao (uk.99).

Riwaya hii inaonekana kuakisi hali halisi ya jamii ya sasa. Hii ni kwa sababu kunao walevi katika jamii ya sasa ambao matendo yao yanalingana na matendo ya wahusika walevi katika riwaya hii. Riwaya hii inaweza kutumika kama kioo cha kumulika yanayotendeka katika jamii ya sasa. Hatua ichukuliwe ili kuiokoa jinsia ya kiume inayopotelea ulevini kwa kukosa matumaini ya kuishi.

**Malezi mabaya**

Katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, kunao wahusika wa kiume ambao wamekosa malezi mazuri. Inaelezwa kuwa, mwanawe Mtemi Lesulia kwa jina Ngoswe alilelewa kwa kuengwaengwa na kudekezwa pamoja na kuhusishwa na ulanguzi wa dawa za kulevya. Ngoswe aliishi maisha ya faiwashi kwenye kasri kubwa peke yake mtaani Majuu. Huyu hakushughulika kujisulubisha na kazi, kwani ndiye aliyekabidhiwa mamlaka ya kukusanya kodi za majimba mengi aliyomiliki mtemi Lesulia. Inaelezwa kuwa, alifuja pesa hizo kwa raha na anasa mbalimbali. Hata zilizomfikia mzazi wake ni chache mno. Aidha, marafiki zake Ngoswe walikuwa wamekataa shule na kuingilia ulanguzi wa dawa za kulevya. Maneno haya yanadhibitisha kuwa wahusika hawa wa kiume hawakupata malezi yanayostahili kutoka kwa wazazi wao. Mwandishi anasema:

> Ngoswe alikuwa mwana kindakindaki, akaengwaengwa na kudekezwa kupita kiasi. Ngoswe alikuwa na marafiki wa kitajiri aliotabaradi nao. Wengi wao walikuwa wamekataa shule, wakaishi kama wafalme kwenye makasri ya wazazi wao. Wengine walikuwa na uraibu wa dawa za kulevya. Aghalabu ndiye aliyezifahamu njia zote za kuzipata dawa hizo (uk. 122).

Kwa sababu ya kukosa malezi mazuri, wahusika hawa wanaingiliana na biashara haramu ya ulanguzi wa dawa za kulevya. Kama anavyoeleza mwandishi, dawa hizo hatari zilisambazwa nchini kwa siri. Mwandishi anasema:

> Ziliuzwa hadi kwenye mitaa duni na mawakala ambao walilipwa na Ngoswe na wenzake (uk. 123).

Aidha, Mangwasha anapokuwa katika ziara zake za kumsaka mumewe mtaani Ponda Mali, anakutana na kundi la vijana ambao walivaa mararu. Kila dalili ilionyesha kwamba hawajaona mlango wa darasa la shule. Kama inavyoelezwa, wengine walikuwa wakivuta vipande vya sigara vilivyotupwa na wapiti njia. Tunaona kuwa, eneo hili lilionekana kukosa maadili mema. Mwandishi kupitia kinywa cha Mangwasha anaandika:

> Walikosa malezi bora ya wazazi wao ambao huenda ni walevi, waliopotelea humo mtaani Ponda Mali. (uk. 35).

Riwaya hii inaonekana kuakisi hali halisi ya jamii ya sasa. Ulanguzi wa dawa za kulevya umekithiri katika jamii ya sasa. Wengi wa wanaolangua dawa hizi ni wanaume.

Nadharia ya uhalisia inadai ya kwamba, fasihi ieleze mambo kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Katika jamii ya sasa, jinsia ya kiume inaathirika kutokana na changamoto ya kutelekezwa katika jamii. Vijana wa kiume wameingilia matumizi mabaya ya vileo na kuwa watu wasioweza kutegemewa maishani. Wamekosa mwelekeo katika maisha yao na kushindwa kuyamudu maisha yao wenyewe. Atieno (2019) anasema ya kwamba, kupuuzwa kwa jinsia ya kiume kumechangia hali yao ya upweke kwani hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike.

Halikadhalika, nadharia ya uhalisia inadai ya kwamba, wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Tunaona kuwa, Ngoswe na wenzake wamechorwa walivyo kulingana na jamii ya sasa. Mtoto anapodekezwa, akikua anafanya mambo ya kuwaumiza wazazi wake na jamii kwa jumla ila wanashindwa kuvisahihisha kwa sababu wanakuwa wameishachelewa. Aidha, jamii ya Matuo ina matukio yanayolingana na hali halisi iliyopo. Mara nyingi, wenye pesa yaani matajiri huwalea watoto wao vibaya na kutumia pesa zao kununua haki. Tunaona kuwa, wakuu wa serikali hawakuwa na uwezo wa kumkamata wala kumshtaki Ngoswe licha ya kuwa mlanguzi wa dawa hatari za kulevya kwa sababu ni mwanawe mtemi.

**Hitimisho**

Katika makala hii tulidhamiria kubainisha changamoto zinazomkabili mhusika wa kiume katika riwaya ya *Nguu za Jadi*. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Imekuwa hali ya mazoea kuona jinsia ya kike ikisawiriwa kwa kiasi kikubwa na kuonyeshwa jinsi inavyoonewa na kudhulumiwa huku jinsia ya kiume ikionekana kama iliyokamilifu, isiyokubwa na matatizo yoyote. Ukweli umebainika kutokana na utafiti huu kuwa, jinsia ya kiume hukubwa na changamoto mbalimbali katika maisha. Changamoto hizo ni pamoja na; ukosefu wa ajira, ukosefu wa elimu, ukosefu wa matumaini, kutelekezwa katika jamii, ulevi wa pombe na malezi mabaya. Hivyo basi jinsia hii inahitaji kutetewa jinsi ambavyo jinsia ya kike hutetewa na jamii.

**MAREJELEO**

Atieno, J. (2019). "Utambulisho wa jinsia katika *Maumbile si Huja* na *Paradiso*." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
Bayyo, F. (2020). "Usawiri wa jinsi ya kiume katika riwaya teule za Shafi Adam Shafi." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa)
Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishers.
Momanyi, C. (2021). *Nguu za Jadi*. Nairobi, Queenex Publishers Limited.
Mulokozi, M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Kauttu publisher: Dar es salaam.
Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele* vyake. Nirobi: Phoenix Publishers Ltd.